**TAARIFA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWA VYOMBO VYA HABARI, KUHUSU ZIARA YA MHESHIMIWA JOKO WIDODO, RAIS WA JAMHURI YA INDONESIA, TAREHE 21 HADI 22 AGOSTI 2023, IKULU, DAR ES SALAAM**

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana:***

Napenda kuchukua fursa hii kukukaribisha tena Mheshimiwa Joko Widodo, Rais wa Jamhuri ya Indonesia na ujumbe wako, katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali na Watanzania wote tumefurahi na tunashukuru kwa heshima uliyotupa kwa kuiweka Tanzania miongoni mwa nchi za Afrika utakazotembelea katika Ziara yako ya kwanza,

tangu uliposhika wadhifa wa Urais **mwezi Oktoba 2014**. **KARIBU SANA!**

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana:***

Uhusiano kati ya Tanzania na Indonesia una historia ndefu iliyoanza na waasisi wa mataifa yetu mawili, Mwalimu Julius Nyerere na Rais Soekarno, tokea wakati wa Mkutano wa Bandung **mwaka 1955**. Tangu wakati huo na kwa miaka mingi, Indonesia imekuwa mshirika mkubwa na wa thamani sana kwa Tanzania. Ni moja kati ya nchi za kwanza kufungua ubalozi kamili hapa nchini mara tu baada ya muungano wetu **mwaka 1964**.

Na baada ya kuanzishwa rasmi kwa mahusiano ya kidiplomasia, nchi zetu mbili zimeendelea kuwa washirika

wenye dhamira na utashi mkubwa wa kuimarisha ushirikiano wetu wa kisiasa na kiuchumi chini ya misingi ya **Azimio la Bandung la 1955**.

Hivyo, wakati wa mazungumzo yetu, mimi na Rais Widodo tumekubaliana kuimarisha urafiki na ushirikiano uliopo katika nyanja za kisiasa, kijamii, na kiuchumi kwa manufaa ya watu wa nchi zetu mbili. Tumebaini kuwa, licha ya uhusiano wetu mkubwa wa kidiplomasia, kuna mengi zaidi yanayoweza kufanyika ili kutumia fursa zilizopo na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano kijamii na kiuchumi.

Tumekubaliana kukuza biashara na uwekezaji kwa kuzileta pamoja sekta za umma na binafsi, yaani *public-public and public-private partnership*. Na hapa, tumedhamiria kuimarisha zaidi ushirikiano wetu katika viwanda, kilimo,

nishati, madini, mafuta na gesi, uvuvi, utalii na sekta ya ukarimu, na kubadilishana maarifa na teknolojia.

Vilevile, wakati wa mazungumzo yetu, nilitoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji uliofanywa na kampuni ya Serikali ya Indonesia, PERTAMINA, katika sekta ya nishati kwenye Gesi Asilia ya Mnazi Bay kule Mtwara. Na nimeukaribisha vyema uamuzi wa PERTAMINA wa kupanua uwekezaji wake katika sekta ya nishati.

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana:***

Nchi zetu mbili zimekuwa zikishirikiana zaidi katika sekta ya kilimo. **Mwaka 1996**, Serikali ya Indonesia ilianzisha Kituo cha Mafunzo ya Kilimo kwa Wakulima Vijijini *(Farmers'*

*Agriculture and Rural Training Centre - FARTC)* kule Mkindo, Morogoro. Kituo kile kimechangia kwa kiasi kikubwa kwenye azma yetu ya kuelimisha wakulima na kutoa mafunzo kwa wataalam wa kilimo. Nimeukaribisha pia uamuzi wa Serikali ya Indonesia wa kufufua shughuli za Kituo hicho.

Ili kufanya ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa maeneo mbalimbali ya ushirikiano, nimemhakikishia Mheshimiwa Rais kuhusu utayari wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mwenyeji wa kikao cha **04** cha Kamati ya Pamoja ya Ushirikiano wa Kilimo (JACC) baadaye mwaka huu.

Aidha, kwa vile Indonesia ni mzalishaji mkubwa zaidi wa mafuta ya mawese duniani, nimemweleza Rais kuhusu

nia ya Tanzania ya kupata uzoefu wa nchi yake katika uzalishaji wa mafuta hayo; na hivyo, kufufua sekta yetu hii. Kama mnavyofahamu, Serikali yetu imejizatiti kuhakikisha tunaongeza uzalishaji wa mafuta ya kula ili tuache kabisa kutumia fedha zetu za kigeni kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi.

Halikadhalika, nimemwomba Mheshimiwa Rais ushirikiano zaidi katika kujenga uwezo na ujuzi wa kiufundi kwenye maeneo yafuatayo;-

i) Mageuzi katika sekta ya Kilimo kwa kutumia teknolojia na zana za kisasa kupitia jukwaa lililopo la Kamati ya Pamoja ya Ushirikiano wa Kilimo (JACC);

ii) Ushirikishwaji wa sekta binafsi katika maendeleo makubwa ya miundombinu;

iii) Uendeshaji wenye tija na ufanisi wa mashirika ya kibiashara yanayomilikiwa na serikali (*State Owned Enterprises - SOEs*). Kama mnavyojua, Indonesia ni kati ya nchi zenye mashirika bora ya kibiashara yanayomilikiwa na serikali, kama vile PERTAMINA;

iv) Kuufanya uchumi wetu kuwa wa kidijitali; na

v) Kuendeleza na Kuongeza Uwezo wetu wa Rasilimali Watu.

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana:***

Katika Ziara hii, tumeshuhudia kusainiwa kwa **Hati 7** za Makubaliano (yaani MoUs) kati ya nchi zetu mbili katika nyanja za Ulinzi; Afya; Biashara; Nishati kwa ngazi ya Wizara, na Mashirika yetu ya Umeme; Kilimo; Uvuvi na Uchumi wa Buluu; Madini; Mifugo; uanzishwa wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano; na Misamaha ya Viza kwa Wamiliki wa Pasipoti za Kidiplomasia na za Huduma.

Ni matumaini yangu ya dhati kwamba, chini ya Makubaliano haya, nchi zetu mbili zitakuwa na sura mpya ya ushirikiano wa kina na mpana zaidi kwa manufaa ya pande zote.

Mbali na masuala ya ushirikiano wa kijamii na kiuchumi, tumebadilishana pia mawazo kuhusu masuala muhimu ya kikanda na kimataifa, na kuthibitisha dhamira yetu ya kusaidiana katika masuala yenye maslahi ya pamoja kwenye nyanja ya kimataifa.